JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2023

# KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU

# DARAJA LA A (GATCE) 2023

# 621 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624, Dar es Salaam,
Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ..... iv
1.0 UTANGULIZI ..... 1
2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ..... 2
2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu) ..... 2
2.1.1 Swali la 1: Stadi za Lugha ..... 2
2.1.2 Swali la 2: Sarufi ..... 4
2.1.3 Swali la 3: Utungaji ..... 7
2.1.4 Swali la 4: Fasihi simulizi ..... 10
2.1.5 Swali la 5: Stadi za lugha ..... 13
2.1.6 Swali la 6: Fasihi simulizi ..... 15
2.1.7 Swali la 7: Utungaji ..... 18
2.1.8 Swali la 8: Vifaa vya mtaala ..... 21
2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili ..... 24
2.1.10 Swali la 10: Upimaji ..... 27
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha ..... 30
2.2.1 Swali la 11: Fasihi simulizi ..... 31
2.2.2 Swali la 12: Sarufi ..... 36
2.2.3 Swali la 13: Maandalizi ya kufundisha ..... 41
2.2.4 Swali la 14: Upimaji ..... 47
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA ..... 51
4.0 HITIMISHO ..... 52
5.0 MAPENDEKEZO ..... 53
KIAMBATISHO CHA PEKEE ..... 54

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limetayarisha taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa cheti daraja la A katika somo la Kiswahili mwaka 2023. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali.

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa cheti daraja la A katika somo la Kiswahili mwaka 2023 inaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kilikuwa kizuri. Ufaulu huo, umechangiwa na watahiniwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa katika mtihani huu na kujibu kwa kufuata matakwa ya maswali yaliyoulizwa, matumizi sahihi ya lugha na alama za uandishi, kutoa hoja sahihi zenye mifano rahisi na kujieleza katika mtiririko unaoleta mantiki. Vilevile, uchambuzi umeonesha kuwa, baadhi ya watahiniwa walipata alama za wastani. Hii imesababishwa na watahiniwa hao kutoa majibu yasiyojitosheleza.

Hata hivyo, watahiniwa wengine walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa, dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili na kujibu kinyume na matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa hao walikosa umahiri wa kujieleza katika mtiririko unaoleta mantiki na kushindwa kuandika sehemu za utangulizi na hitimisho hususani katika maswali ya insha.

Baraza linatarajia kuwa, taarifa hii itawawezesha walimu tarajali na wakufunzi kuelewa sababu za watahiniwa kujibu au kutokujibu vizuri maswali mbalimbali. Hivyo, itawasaidia kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na utunzi wa mitihani katika ngazi ya chuo ili kufanya vizuri zaidi katika mitihani ijayo inayotolewa na Baraza la Mitihani.

Baraza la mitihani linatoa shukrani kwa wadau wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Kiswahili ulifanyika mwezi Mei, 2023 ambapo ulitungwa kwa kuzingatia muhtasari wa Taaluma na Utaalamu wa kufundisha Kiswahili ngazi ya cheti daraja la A wa mwaka 2009. Mtihani huu ulikuwa na maswali 14 yaliyogawanyika katika sehemu mbili ambazo ni A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ya majibu mafupi na sehemu B ilikuwa na maswali manne (4) ya insha. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A na B. Katika sehemu A kila swali lilikuwa na alama 4 na kufanya jumla ya alama 40 ambapo sehemu B kila swali lilikuwa na alama 15 na kufanya jumla ya alama 60.

Ufaulu wa watahiniwa umegawanyika katika viwango vitatu ambavyo: kiwango kizuri (asilimia 70 hadi 100), kiwango cha wastani (asilimia 40 hadi 69) na kiwango hafifu (asilimia 0 hadi 39). Aidha, chati za viwango vya ufaulu kiasilimia zimebainishwa katika kila swali. Viwango vya ufaulu wa watahiniwa vimeainishwa kwa kutumia rangi tatu ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na rangi nyekundu ufaulu hafifu.

Jumla ya watahiniwa 5,117 walisajiliwa kufanya mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2023. Miongoni mwao, watahiniwa 5,078 ambao ni sawa na asilimia 99.23 ya watahiniwa waliosajiliwa walifanya mtihani. Hata hivyo, watahiniwa 39 (0.77%) hawakufanya mtihani. Aidha, watahiniwa 5,020 (99.88%) walifaulu.

Takwimu hizo zinadhihirisha kwamba, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika mtihani huu ni kizuri. Hata hivyo, kiwango hiki kimeshuka kwa asilimia 0.12 ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu.


## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu)

Swali litakuwa limejibiwa vizuri ikiwa theluthi mbili (2/3) na zaidi ya watahiniwa watakuwa wamepata alama 2-4 na litakuwa limejibiwa vibaya ikiwa theluthi mbili (2/3) na zaidi ya watahiniwa ndio waliopata alama 0-1.5. Aidha, swali litakuwa limejibiwa kwa kiwango cha wastani ikiwa idadi ya watahiniwa waliopata alama 2.0-2.5 inazidi theluthi moja (1/3) na haikuzidi theluthi mbili (2/3).


#### 2.1.1 Swali la 1: Stadi za Lugha

Swali lilimtaka mtahiniwa kuainisha mazoezi manne yanayoweza kukuza stadi ya Kuandika. Watahiniwa 5,078 sawa na asilimia 100 waliofanya mtihani, walijibu swali hili ambapo asilimia 63 walipata alama 2 hadi 4 na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani kama inavyoonekana katika chati Na. 1.




**Chati Na. 1**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 3,199, sawa na asilimia 51.2, walipata alama 3 hadi 4 kwa kuwa waliweza kuainisha kwa usahihi aina 3 hadi 4 za mazoezi yanayoweza kukuza stadi ya kuandika. Kwa mfano, mtahiniwa aliyepata alama 3 kati ya 4 alitoa majibu yafuatayo: *(a) Kuwaelekeza na kuwafundisha wanafunzi taratibu za uandishi (b) Kuwapa wanafunzi kazi zenye kuhitaji kuandika (c) Kuwapa mazoezi mengi ya ufupisho wa habari ili kubaini mawazo makuu na kuweza kuimarisha stadi zao za kuandika maandishi (d) Kupima uwezo wa wanafunzi katika kusoma ili uweze kubaini kama wana changamoto ya kutojua kusoma.* Majibu ya vipengele (a), (b) na (c) ni sahihi wakati katika kipengele (d) jibu siyo sahihi. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeainisha kwa usahihi mazoezi yanayoweza kukuza stadi ya kuandika.



1

i/- Kuwasomea imla; imla itawasaidia katika kukuza stadi ya kuandika na kufahamu maneno mbalimbali.

ii/- Kuwapatia nukuu. Baada ya kufundisha nitawapatia nukuu ili wazoee kuandika mara kwa mara.

iii/- Kuwapa zoezi la kujaza fomu. kujaza fomu kutawasaidia pia kukuza stadi ya kuandika.


iv/- kuwapa zoezi la kuandika barua. Nitahakikisha nawapatia zoezi hili ili waweze kuwa na ujuzi wa namna ya kuandika barua lakini pia itawasaidia kukuza stadi ya kuandika.

**Kielelezo Na. 1.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1.

Hata hivyo, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 1,879, sawa na asilimia 37 ya waliojibu swali hili, walikuwa na uelewa mdogo wa mazoezi yanayoweza kukuza stadi ya Kuandika hivyo kupata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa wengine waliandika majibu yasiyokidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya mbinu za kufundishia na kujifunzia stadi za kuandika na kusoma kama ifuatavyo: *Kuandika chini, kutafuta majarida mbalimbali, kuwapa vitabu vya kiada ili kuwafanya waweze kusoma na kutumia kadi za namba.*

Zaidi ya hayo mtahiniwa mwingine aliandika hatua za ufundishaji na ujifunzaji darasani kama ifuatavyo: *kuandika neno ubaoni, kuwaongoza wanafunzi wasome kwa pamoja, kumtaka kila mwanafunzi mmoja mmoja kusoma, kuwaongoza kuandika maneno katika daftari.*

Watahiniwa wengine walitoa majibu ya namna watakavyowapima wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mtahiniwa mmoja aliandika majibu yafuatayo: *usomaji wa imla, kuwapa mazoezi ya kutosha, kazi mradi na kazi za nyumbani.* Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuainisha mazoezi anayoweza kutumia kwa ajili ya kukuza stadi ya kuandika.


1 (i) ~~Stadi~~
(i) kusoma
(ii) kuandika
(iii) kusikiliza
(iv) kuzungumza.

**Kielelezo Na.1.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1.


Katika kielelezo Na.1.2, mtahiniwa alitaja stadi nne za lugha badala ya kuainisha mazoezi manne atakayotumia kukuza stadi ya kuandika.

Kwa upande mwingine uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 599, sawa na asilimia 11.8 ya waliojibu swali hili, walikuwa na ufaulu wa wastani, kwa kuwa walipata alama 2.0 hadi 2.5. Baadhi yao walitaja hoja mbili sahihi na nyingine mbili zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *(a) Kuwapa mazoezi ya uandishi wa Makala mara kwa mara (b) Kuwafundisha jinsi ya kuzingatia alama za uandishi wakati wa kuandika, mfano alama za nukta (c) Kuwaongoza wanafunzi kuzingatia matumizi sahihi ya msamiati ili kupata maana ya ujumbe wake (d) Kurekebisha matatizo ya ala katika kutamka ili wasiziandike kama wanavyotamka mfano. Rara badala ya lala.* Vipengele (a) na (b) ni majibu sahihi wakati (c) na (d) siyo majibu sahihi.

### 2.1.2 Swali la 2: Sarufi


Swali lilimtaka mtahiniwa abainishe kauli ya utendaji inayowakilishwa katika sentensi alizopewa. Watahiniwa 5,078, sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani, walijibu swali hili ambapo

asilimia 63.2 walipata alama 2 hadi 4 na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani kama inavyoonekana katika chati Na. 2.




**Chati Na. 2**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 3,092, sawa na asilimia 60.9, waliweza kubainisha kauli za utendaji katika sentensi walizopewa na kupata alama 3 hadi 4. Miongoni mwao, watahiniwa 2,476, sawa na asilimia 48.8, walifanya vizuri sana na kupata alama zote nne (4). Kwa mfano, wanafunzi hao walibainisha kauli ya utendaji katika kipengele cha (i) sentensi *Mgala anaimba wimbo* kuwa *kauli ya kutenda*, (ii) sentensi *Baba aliitwa shuleni* kuwa *kauli ya kutendwa,* (iii) sentensi *Maji yalimwagika ndani* kuwa *kauli ya kutendeka* na (iv) sentensi *Juma na John wanapigana* kuwa *kauli ya kutendana/kutendeana*. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha kwa usahihi kauli za utendaji katika sentensi zote alizopewa.


2
(a) kauli ya kutenda.
(b) kauli ya kutendwa
(c) kauli ya kutendeka.
(d) kauli ya kutendeana.


**Kielelezo Na. 2.1**: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,833, sawa na asilimia 36.1, walishindwa kubainisha kauli za utendaji kwenye sentensi walizopewa katika vipengele vyote vinne na kupata alama 0. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kubainisha kauli za utendaji katika sentensi mbalimbali. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alinakili vitenzi kutoka kwenye sentensi alizopewa na kutoa majibu kama ifuatavyo: (a) *Mgala anaimba wimbo - jibu anatenda au kutenda- Anaimba, (b) Baba aliitwa shuleni, –jibu Aliitwa, (c) Maji yalimwagika, jibu–Yalimwagika, (d) Juma na John wanapigana, jibu– Wanapigana.*

Mtahiniwa mwingine aliondoa viambishi nafsi na vya wakati kutoka kwenye vitenzi vya sentensi alizopewa na kuandika kama ifuatavyo: *(a) Imba (b) Ita (c) Mwaga (d) Piga.*

Baadhi ya watahiniwa walichanganya kati ya dhana ya kauli za utendaji na zile za kauli halisi na kauli taarifa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *kauli halisi na kauli taarifa*.

Vilevile watahiniwa wengine walinakili sentensi walizopewa katika swali hili na kuziandika bila kubainisha kauli za utendaji kama inavyoonekana katika majibu yafuatayo ya mtahiniwa mmoja: *(a) Mgala anaimba wimbo (b) Baba aliitwa shuleni (c) Maji yalimwagika ndani (d) Juma na John wanapigana*. Majibu hayo ya watahiniwa yanadhihirisha kuwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha katika kauli za utendaji. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha kwa usahihi kauli za utendaji zinazowakilishwa katika sentensi alizopewa.


2 Bainisha kauli ya utendaji katika sentensi zifuatazo

(a) Ngala, anaimba wimbo
anaimba

(b) Baba aliitwa shuleni
aliitwa

(c) Maji yalimwagika ndani
yalimwagika

(d) Juma na John wanapigana
wanapigana


**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 2.

Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebainisha vitenzi katika sentensi alizopewa badala ya kubainisha kauli za utendaji wa vitenzi hivyo katika sentensi.

Aidha, watahiniwa 115, sawa na asilimia 2.3, walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu. Watahiniwa hao waliweza kubainisha kwa usahihi kauli za utendaji katika sentensi mbili kati ya nne, hivyo kupata alama 2. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yafuatayo: (*a) Ni kauli ya kutenda (b) Ni kauli halisi (c) Ni kauli ya kutendewa (d) Ni kauli ya kutendeana.* Majibu katika vipengele (a) na (d) yalikuwa sahihi wakati (b) na (c) hayakuwa sahihi. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na ujuzi wa wastani katika mada ya kauli za utendaji.


### 2.1.3 Swali la 3: Utungaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua kwa ufupi vigezo vinne vitakavyomuongoza kumbaini mshindi katika mashindano ya uandishi wa insha. Swali lilijibiwa na watahiniwa 5,078, sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango kizuri kwani asilimia 98.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 3 inafafanua viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 3:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 4,386, sawa na asilimia 86.4, walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu huo ulitokana na uelewa mkubwa waliokuwa nao juu ya mada ya *Utungaji*. Hivyo, waliweza kuchambua kwa ufupi vigezo vinne vitakavyowaongoza kumbaini mshindi wa insha. Vigezo hivyo ni: *Matumizi ya lugha fasaha, Matumizi sahihi ya alama mbalimbali za uandishi, Mpango wa mawazo na mantiki yake, Kuzingatia kichwa cha habari, Kuandika utangulizi unaovutia umakini wa wasomaji na wasikilizaji, Kuandika kiini cha insha kwa mpangilio unaofaa, Kuandika mwisho wa insha unaovutia na kutoa hitimisho.* Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyeweza kuchambua kwa ufupi vigezo vinne vitakavyomuongoza kumbaini mshindi wa insha.



3
i) Kuchunguza kama ame andika kichwa cha insha
ii) kubaini / kuchunguza kama ameandika utangulizi katika insha kwa usahihi
iii) Kuchunguza kama ameandika kiini cha insha
iv) Kuchunguza/kuangalia kama ame andika Hitimis ho au Mwisho wa insha Nizuri

**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 621, sawa na asilimia 12.2, walipata alama 2 hadi 2.5. Baadhi yao walitaja hoja mbili sahihi na hoja nyingine zisizo sahihi, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yafuatayo: *(a) Matumizi bora ya alama za uandishi (b) mpangilio mzuri wa maudhui (c) Jinsi alivyohusianisha na mazingira yanayomzunguka (d) Kiasi cha maarifa waliyo nayo kuhusiana na athari za madawa ya kulevya*. Majibu hayo ya mtahiniwa yalikuwa sahihi katika vipengele (a) na (b) wakati (c) na (d) hayakuwa sahihi. Watahiniwa wengine waliandika hoja nne bila kufafanua kwa ufupi, hivyo kupata alama 0.5 kwa kila hoja, mfano mtahiniwa mmoja aliandika: *Kichwa cha insha, Utangulizi wa insha, Kiini cha insha, Hitimisho.*

Kwa upande mwingine watahiniwa 71, sawa na asilimia 1.4, walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao walishindwa kuchambua kwa ufupi vigezo vinne vya kuwaongoza kumbaini mshindi wa insha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zinazohusiana na athari za madawa ya kulevya badala ya vigezo atakavyotumia kumpata mshindi wa insha kama ifuatavyo: *Athari za madawa ya kulevya, Kusababisha umaskini, Kupelekea watu kuwa maskini na Ongezeko la watoto wa mitaani.*

Zaidi ya hayo, watahiniwa wengine walipendekeza mazoezi ya kukuza stadi ya Kuandika badala ya vigezo vitakavyowaongoza kumpata mshindi wa uandishi wa insha. Mtahiniwa mmoja aliandika majibu kama vile: *(a) Kuwapa mazoezi mengi ya kuandika (b) kuwashirikisha katika shughuli nyingi za utungaji (c) Kutoa motisha (d) Kutoa mashindano ya uandishi mara kwa mara.* Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuchambua kwa ufupi vigezo vinne vitakavyomuongoza kumbaini mshindi wa uandishi wa insha.




3 (i) Kubaini wahusika kwanza.
(ii) Kutunga shera kali mayowakata kutumia madawa ya kulevya.
(iii) Kutoa elimu au kuwaelimisha juu ya madhara ya kutumia madawa ya kulevya.
(iv) Kuhakikisha hakuna mtumiaji wa hayo madawa tena.

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

Katika kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa alipendekeza njia za kuondokana na tatizo la dawa za kulevya badala ya kuchambua kwa ufupi vigezo vinne vitakavyomuongoza kumbaini mshindi wa uandishi wa insha.

### 2.1.4 Swali la 4: Fasihi Simulizi


Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha, kwa kutumia hoja nne, kuwa nahau ni semi zenye umuhimu katika lugha na jamii. Watahiniwa 5,078 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa, kwani watahiniwa sawa na asilimia 98.6 walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa.




**Chati Na. 4:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4

Watahiniwa 4,599, sawa na asilimia 90.6, walijibu swali hili vizuri na kupata alama 3 hadi 4 kwa kuwa walikuwa na uelewa

wa kutosha katika *Fasihi Simulizi*. Watahiniwa hao, waliweza kuthibitisha kwa kutumia hoja sahihi 3 hadi 4 kuwa Nahau ni semi zenye umuhimu katika lugha na jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama vile: *Huelimisha, Hukosoa jamii, Hukuza msamiati, Hulinda utamaduni wetu*. Aidha watahiniwa waliopata alama 3 walitoa majibu kama vile: *(a) Hukuza lugha (b) Huonya jamii (c) Huficha maana ya kitu hivyo huhitaji hekima kufumbua (d) Hukutanisha watu katika jamii*. Jibu katika kipengele (d) ndiyo peke yake halikuwa sahihi. Kwa ujumla, watahiniwa wa kundi hili walikuwa na umahiri na mawanda mapana kuhusu mada ya *Fasihi simulizi*. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyeweza kuthibitisha kwa kutumia hoja nne kuwa nahau ni semi zenye umuhimu katika lugha na jamii.



4
i) Husaidia kukuza lugha husika.
ii) Husaidia kupunguza Ukali wa maneno yanayotamkwa.
iii) Nahau Hutoa Maana ya Maneno kwa kutumia lugha ya kuficha /Picha.
iiii) Huweza kuelimisha Jamii

**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 4.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 406, sawa na asilimia 8.0, walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya *Fasihi Simulizi*, hivyo waliweza kuthibitisha umuhimu wa nahau katika lugha na jamii kwa kutoa hoja mbili sahihi kati ya nne. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yafuatayo: (a) *Nahau hupendwa na kuzungumzwa na kila rika (b) Nahau hutumia lugha za mficho ili kupunguza ukali maneno (c) Nahau huwa na wahusika wawili mfano anayetoa nahau na anayejibu (d) Nahau huburudisha na kuonya jamii.* Katika majibu haya hoja katika vipengele (b) na (d) zilikuwa sahihi ilhali kwenye vipengele (a) na (c) hazikuwa sahihi.

Hata hivyo, watahiniwa 73, sawa na asilimia 1.4, walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha

katika mada ya *Fasihi Simulizi* kwa kuwa walishindwa kutoa hoja zinazothibitisha umuhimu wa nahau katika lugha na jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yasiyohusiana na matakwa ya swali: *Nahau nomino, Nahau kitenzi, Nahau kielezi na Nahau kivumishi*. Watahiniwa wengine hawakuelewa matakwa ya swali kwani badala ya kuthibitisha kwa kutumia hoja nne kuonesha umuhinu wa nahau katika lugha na jamii, watahiniwa hao walijibu kwa kuandika nahau na maana zake, kama vile: *(a) Kata shauri = Amua kufanya jambo (b) Piga moyo konde = Kukubaliana jambo (c) Kufa kishujaa= Kufa kwa kupigana vitani (iv) Tia nanga = Kufika mwisho.* Hali kadhalika, watahiniwa wengine waliandika methali na kutoa maana zake. Mathalani, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yafuatayo: *(a) Hakiba haiozi = Tunajifunza kuweka hakiba ili itusaidie baadaye (b) Halaka halaka haina Baraka = Tunajifunza tusiwe na maamzi ya haraka tupatwapo na shida (c) Usipoziba ufa utajenga ukuta (d) Baniani mbaya kiatu chake dawa.* Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa mmojawapo.



4
5. (i) Kuwa na utayari wa kusikiliza; wanafunzi wataki wa kujiweka tayari ili kusikiliza kutakacho elezwa,
(ii) Kuepuka vikwazo vya usikivu; mfano kupiga kelele, kutembea darasani, na kuongea.
(iii) Kuandika dondoo (nukuu muhimu); wanapo sikiliza ni muhimu kuandika wanacho kiona ni cha muhimu ili wasi sahau.
(iv) Kuuliza maswali pale wasipo elewa, na kusikiliza kwa umakini, wanafunzi wanatakiwa kusikiliza kwa umakini na kuuliza maswali wasipo elewa ili waelewe zaidi.

**Kielelezo Na. 4.2**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4.

Katika kielelezo Na. 4.2, mtahiniwa aliandika mambo ya kuzingatia katika stadi ya kusikiliza badala ya kuthibitisha kuwa nahau ni semi zenye umuhimu katika lugha na jamii.

### 2.1.5 Swali la 5: Stadi za Lugha

Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja mambo manne ya kuzingatia katika mchakato wa kusikiliza hadithi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5,078 sawa na asilimia 100. Kati yao, asilimia 59.8 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4 na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa.





**Chati Na. 5:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5

Watahiniwa 2,394, sawa na asilimia 47.1, walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwani walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao waliweza kutaja mambo mawili kwa usahihi kati ya manne ambayo wanapaswa kuzingatia wakati wa kusikiliza hadithi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yafuatayo: *(a) Kuzingatia mkao mzuri wakati wa masimulizi baina ya msikilizaji na msimuliaji (b) Kuhakikisha utulivu baina ya msikilizaji (c) Kuwepo kwa uhusiano mzuri baina ya msikilizaji na msimuliaji (d) Kuandika au kunukuu mambo muhimu yatakayozungumzwa katika hadithi hiyo.* Majibu katika vipengele (b) na (d) ni sahihi lakini katika kipengele (a) na (c) siyo sahihi. Majibu hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya stadi ya kusikiliza.

Aidha, watahiniwa 2,039, sawa na asilimia 40.2, waliofanya swali hili, walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu stadi ya kusikiliza na hasa

mambo ya kuzingatia wakati wa kusikiliza hadithi. Hivyo, walishindwa kutaja mambo hayo kwa usahihi. Kwa mfano, baadhi yao walitoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *Namna au njia zilizotumika Tanzania kupata uhuru, matokeo baada ya kupata uhuru, faida za kupata uhuru, Kiongozi aliyedai uhuru na wakoloni waliokuwa wanatawala.* Watahiniwa wengine waliandika dondoo kuonesha mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika insha. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *Lazima kuzingatia kichwa cha habari, Lazima kuzingatia mwanzo au utangulizi wa hadithi, Lazima kuzingatia kiini cha hadithi kwa kufuata mtiririko mzuri wa mawazo, Lazima kuzingatia mwisho au hitimisho wa hadithi*. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutaja mambo manne ya kuzingatia wakati wa kusikiliza hadithi.



5
i) Kiongozi aliyepambana au aliyepigania Uhuru.
ii) Mambo yaliyofanyika mpaka tukapata Uhuru.
iii) Njia zilizotumika kupata Uhuru.
iv) kwanini tunasema Tanzania ni nchi ya Uhuru au Sababu zilizopelekea Uhuru.

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.

Kielelezo Na. 5.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyeandika dondoo kuonesha Tanzania ilivyopata uhuru badala ya mambo manne ya kuzingatia wakati wa kusikiliza hadithi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 645, sawa na asilimia 12.7, walijibu swali hili na kupata alama 3 hadi 4. Ufaulu huo unatokana na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Stadi za lugha* hususani katika mada ndogo ya *stadi ya kusikiliza*. Hivyo, waliweza kubainisha kwa usahihi mambo manne ya kuzingatia wakati wa kusikiliza hadithi. Watahiniwa hao waliweza kutaja mambo kama vile: *Lazima wasikilizaji wawe na utulivu ili waweze kusikia kwa usahihi, lazima waweze kubaini dhamira kuu katika masimulizi, lazima wazingatie matumizi ya lugha ili waelewe mfano tamathali za semi , lazima wazingatie*


*alama za uandishi mfano kituo au mkato*. Majibu hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa mkubwa na mawanda mapana katika *Stadi za lugha* hususani kwenye mada ndogo ya *stadi ya kusikiliza*. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha kwa usahihi mambo manne ya kuzingatia wakati wa kusikiliza hadithi.


5
i) Kuwa wasikivu na kuweza kusikiliza kinacho simuliwa
ii) Kumwangalia Msimuliaji
iii) Kubaini ujumbe uliopo kwenye hadithi
iv) Kuhusisha jambo alilolisikia na jambo alilowahi kusikia

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5.

### 2.1.6 Swali la 6: Fasihi Simulizi


Swali lilimtaka mtahiniwa abainishe methali zinazowakilishwa na maana alizopewa katika sentensi. Watahiniwa 5,078, sawa na asilimia 100, walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu, kwani asilimia 76.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Watahiniwa 2,278, sawa na asilimia 44.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walipata alama 2 hadi 2.5 kutokana na uelewa wa wastani waliokuwa nao katika mada ndogo ya *Methali*. Watahiniwa wa kundi hili walifanikiwa kubainisha methali mbili kati ya nne, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha methali zifuatazo: *(a) Mtaka cha uvunguni sharti ainame (b) Akiba haiozi (c) Kelele za chura hazimnyimi tembo kunywa maji (d) Mchumia juani hulia kivulini*. Methali katika vipengele (b) na (d) zilikuwa sahihi wakati (a) na (c) hazikuwa sahihi.

Vilevile watahiniwa 1,585, sawa na asilimia 31.2, waliojibu swali hili walipata alama 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ndogo ya *Methali*. Watahiniwa hao waliweza kubainisha methali zinazowakilisha maana zilizotolewa katika swali. Majibu yaliyotolewa na watahiniwa hao ni pamoja na: *Aisifuye mvua imemnyea, Akiba haiozi, Akili nyingi huondoa maarifa, Baada ya dhiki faraja*. Katika kundi hili, wapo watahiniwa ambao walibainisha methali tatu sahihi badala ya nne na hivyo kupata alama 3. Mathalan, mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *(a) Aisifuye mvua imemnyea (b) Akiba haiozi (c) Mtaka yote kwa pupa hukosa yote (d) Mchumia juani hulia kivulini/Baada ya dhiki faraja.* Majibu katika vipengele (a), (b) na (d) ni sahihi wakati jibu la kipengele (c) siyo sahihi. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha methali zinazowakilisha maana zilizotolewa katika swali.


6 (a) Aisifuye mvua imemnyeshea.
Huwezi ukasifia kitu ambacho hukijui au hujawahi kukiona na kuona faida au madhara yake.

(b) Akiba haiozi. kitu ambacho kimewekwa kwa manufaa ya badae hakiwezi kuharibika kwani kitasaidia baada ya kuwepo kwa uhitaji.


(c) Akili nyingi huondoa maarifa
Ni kile kitendo cha kujiweka ujanja kila kitu mwisho we unaharibu

(d) Mchumia juani hulia kivulini.
Hii ni kusamba mtu yeyote huweza kuhangaika sana lakini kwa baadaye huweza kupata matunda yake na kuishi vizuri kama mfalme.

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,215, sawa na asilimia 23.9 ya waliojibu swali hili, walipata alama 0 hadi 1.5 kwa sababu walikuwa na uelewa mdogo kuhusu mada ndogo ya *Methali*. Watahiniwa hao walishindwa kubainisha methali zinazowakilisha maana zilizotolewa katika swali. Miongoni mwao walitoa majibu tofauti na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kama ifuatavyo: *Chanda chema huvikwa pete: Kuwakilisha maana ya mtu anayeweza kukisifu kitu au kukielezea uzuri wake ni aliyefaidika kutokana na kitu hicho, Akiba haiozi: kuwakilisha maana ya kuwa kitu kilichowekwa au kuhifadhiwa huweza kumfaa mtu wakati wa shida, Asiyesikia la mkuu huvunjika guu: kuwakilisha maana ya mtu anayejiona kuwa ni mwerevu huweza kuondoa busara aliyo nayo na kuharibu aliyoyafanya, na Mtaka cha uvunguni sharti ainame: kuwakilisha maana ya furaha na raha huja baada ya taabu nyingi.* Mtahiniwa hakuelewa matakwa ya swali, kwani badala ya kubainisha methali za maana alizopewa, mtahiniwa alitunga methali na kutoa maana zake.

Aidha watahiniwa wengine katika kundi hili walibainisha aina za sentensi badala ya methali zinazowakilishwa na maana zilizotolewa katika swali. Mathalani, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama vile: *Sentensi changamano, Sentensi sahili, Sentensi shurutia, Sentensi shurutia.* Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali hili.



6 Methali zinazowakilishwa katika maan
(a) Mtu anayeweza kukisifu kitu au kukielezea
uzuri wake ni aliyefaidika kutokana
na kitu hicho.
⇒ Uzuri wake
(b) Kitu kinachowekwa au kuhifadhiwa
kuweza kumfaa mtu wakati wa shida.
⇒ Kidogo kidogo, hujaza buyu la asali.
(c) Mtu anapojiona kuwa ni mwerevu sana
huweza kuonekana kuwa aliyoneyo na kuharibu
aliyofanya.
⇒ Kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza.
(d) Furaha na raha huja wakati wa taabu.
⇒ Mtaka cha mvunguni sharti ainame.

**Kielelezo Na. 6.2**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 6.

Kielelezo Na.6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa maana na kuandika methali zake badala ya kubainisha methali zinazowakilisha maana zilizotolewa katika swali.


## 2.1.7 Swali la 7: Utungaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi sifa nne za barua atakayoandika katika gazeti la Mwananchi ili jamii itambue umuhimu wa kuweka mazingira katika hali ya usafi. Swali lilijibiwa na watahiniwa 5,078 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwani ni asilimia 15.8 tu ya watahiniwa waliojibu swali hili ndiyo walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 7 inafafanua viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Zaidi ya robo tatu ya watahiniwa (4,278), sawa na asilimia 84.2 ya waliofanya swali hili, walipata alama 0 hadi 1.5 kutokana na uelewa mdogo waliokuwa nao katika mada ya *Utungaji*. Watahiniwa hao walishindwa kueleza kwa ufupi sifa nne za barua watakayoandika katika gazeti la Mwananchi ili jamii itambue umuhimu wa kuweka mazingira katika hali ya usafi. Kwa mfano, baadhi yao waliandika mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha kama vile: *sifa zinazotakiwa kuwepo katika barua za magazetini ni kichwa cha habari, utangulizi, kiini cha barua na hitimisho.* Aidha watahiniwa wengine waliandika dondoo watakazotumia kwenye uandishi wa insha kuhusu umuhimu wa kuweka mazingira katika hali ya usafi. Mathalani, mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *Kueleza athari za mazingira machafu, Kutoa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira, Umuhimu wa utunzaji mazingira, Jinsi na namna ya kuweka mazingira katika hali ya usafi*. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa ufupi sifa zinazotakiwa katika barua za magazetini.





**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7.

Kielelezo Na. 7.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyetoa mapendekezo ya namna ya kuepukana na mazingira machafu badala ya kueleza kwa ufupi sifa nne zitakazokuwepo katika barua atakayoandika kwenye gazeti la Mwananchi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 658 (13.0%) walipata alama 2 hadi 2.5 kwa kuwa walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya *Utungaji*. Baadhi yao walieleza kwa ufupi hoja mbili sahihi kati ya nne, hivyo kupata alama 2. Majibu yaliyotolewa na mmoja wa watahiniwa hao ni pamoja na: (a) *Azingatie alama za uandishi (b) Azingatie matumizi sahihi ya lugha fasaha (c) Azingatie mpangilio mzuri mawazo yake wakati wa uandishi (d) Aweze kubainisha ujumbe wake kwa wananchi wenzake.* Majibu hayo ni sahihi katika vipengele (b) na (c) wakati (a) na (d) siyo sahihi. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja mbili sahihi na nyingine moja isiyojitosheleza, hivyo kupata alama 2.5.

Aidha, watahiniwa 142, sawa na asilimia 2.8, walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao, walikuwa na umahiri wa kutosha katika mada ya *Utungaji* kwa sababu waliweza kueleza kwa ufupi sifa tatu hadi nne zinazotakiwa kuwepo kwenye barua katika gazeti la Mwananchi. Baadhi ya watahiniwa walitoa majibu kama vile: *Barua iwe fupi na yenye ujumbe uliokamilika, lugha fasaha na sanifu, maelezo yenye hoja zenye uthibitisho wa kutosha na pia barua kuwa na anwani, sahihi na jina kamili la mwandishi.*

Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja sifa zinazotakiwa katika barua ya magazetini.


7

i) Iwe fupi na wazi kwa kawaida barua za Magazeti zinapaswa kuwa wazi kwa Msomaji.

ii) Itumie Lugha Sanifu na Fasaha, pia lugha inayotumika iwe ni Lugha inayoeleweka kwa jamii husika.


iii) Iwe na Lengo au dhumuni pia barua hizi za Magazeti zinatakiwa kuwa na kusudi au lengo la barua hiyo

iv) jina na Saini ya Mwandishi pia barua za Magazeti zinapaswa kuwa na jina pamoja na saini ya Mwandishi.

**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7.

### 2.1.8 Swali la 8: Vifaa vya Mtaala

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi faida nne atakazozipata mwalimu iwapo atatumia kitabu cha ziada kufundishia somo la Kiswahili. Watahiniwa 5.078, sawa na asilimia 100, walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu, kwani asilimia 97.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 4,367, sawa na asilimia 86.0, walijibu swali hili na kupata alama 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya *Vifaa vya Mtaala*. Watahiniwa hao waliweza kueleza faida tatu mpaka nne za kutumia kitabu cha ziada. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza faida hizo kuwa ni*: Kujipatia maarifa ya ziada, kupata maelezo ya zaidi kuhusiana na mada mbalimbali, kupata mada mbalimbali ambazo hazikuoneshwa katika kitabu cha kiada na pia kujiamini wakati wa ufundishaji.* Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa mmojawapo.


**8** (i) Inamsaidia mwalimu kujiongezea maarifa juu ya swala analoenda kufundisha mfano kwenye kitabu cha kiada kuna mada ya ufugaji bora wa ngombe wa maziwa katini hakina aina za ngombe wa maziwa lakini kwenye kitabu cha ziada kina aina za ngombe wa maziwa.
(ii) Inamsaidia mwalimu kufundisha kwa kujiamini bila ya kubabaika au kubahatisha kwa sababu amepitia vitabu mbali katika kukamilisha somo lake vizuri.
(iii) Inamsaidia mwalimu kuwapatia wanafunzi taarifa ya rejea mbalimbali zinazoendana na somo analofundisha ili wanafunzi wakatafute wasome ili kujiongezea maarifa zaidi.
(iv) Inamsaidia mwalimu kuwapa wanafunzi upeyanuzi wa kiwango cha juu cha mada mfano katika kitabu cha kiada kina labda mada ya aina za maneno tu kwa kutaja lakini kitabu cha kiada kina aina za maneno pamoja na maelezo yake.

**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 8.

Vilevile, watahiniwa 597, sawa na asilimia 11.8, waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 2.5 kutokana na uelewa wa wastani waliokuwa nao katika mada ya *Vifaa vya Mtaala*. Baadhi yao, walibainisha hoja nne sahihi bila kueleza kwa ufupi kama yalivyokuwa matakwa ya swali, hivyo kupata alama 2. Wengine walieleza hoja mbili kwa usahihi kama vile: *(a) Kumsaidia mwalimu kupata ujuzi na maarifa zaidi kuhusu somo lake la Kiswahili (b) kinamsaidia mwalimu kuwa na uelewa mkubwa kuhusu somo lake (c) kinamsaidia mwalimu kupata mbinu mbalimbali za kufundisha somo lake (d) humsaidia mwalimu kukuza stadi ya udadisi na ubunifu katika somo lake.* Katika

majibu hayo kipengele (a) na (b) ni sahihi ilhali (c) na (d) siyo sahihi.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (114) sawa na asilimia 2.2 walipata alama 0 hadi 1.5 kwa sababu walikuwa na uelewa mdogo katika mada ya *Vifaa vya Mtaala*. Watahiniwa hao walishindwa kueleza kwa ufupi manufaa atakayopata mwalimu ikiwa atatumia kitabu cha ziada kufundisha somo la Kiswahili. Katika kundi hili, baadhi ya watahiniwa waliandika hoja moja sahihi na kupata alama 1. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa: *(a) kitabu cha ziada humsaidia mwalimu kupata maarifa ya ziada (b) humsaidia mwalimu na mwanafunzi kuwa na kumbukumbu za muda mrefu (c) humsaidia mwanafunzi kuwa na ari na saikolojia ya kulipenda somo (d) kumsaidia mwanafunzi kuwa mdadisi katika tendo la kujifunza*. Katika majibu hayo, hoja katika kipengele (a) ni sahihi ila majibu katika vipengele (b), (c) na (d) siyo sahihi kwa sababu yanahusu manufaa ya kutumia mbinu shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji. Aidha watahiniwa wengine hawakuelewa matakwa ya swali na kuandika hoja zinazohusiana na mambo ya kuzingatia katika lengo mahususi. Mathalani, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yafuatayo: *Lengo mahususi lazima liwe na vitenzi vinavyopimika, mfano taja, eleza, tofautisha, orodhesha na fupisha, Lengo mahususi lazima liwe na muda, mfano ndani ya kipindi cha dakika 40 kila mwanafunzi aweze kutaja stadi nne za lugha, Lengo mahususi limtaje mlengwa; Mlengwa katika lengo mahususi ni mwanafunzi, Lengo mahususi lazima lifikike na pia lisiwe na malengo mahususi mengi, mfano baada ya kipindi cha dakika arobaini kila mwanafunzi aweze kutaja aina tatu za maneno ni lazima lengo mahususi lifikiwe*. Majibu hayo, yanadhihirisha kuwa watahiniwa wa kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Vifaa vya Mtaala*. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza manufaa ya kitabu cha ziada.




8 manufaa ya kitabu cha ziada.
(i) humwonesha mwalimu mpangilio mzuri wa mada.
(ii) humsaidia mwalimu kujua mbinu bora na zana za kufundishia na kujifunzia
(iii) humsaidia mwalimu kubaini shughuli za utendaji darasani
(iv) humsaidia mwalimu kujiamini darasani kwa sababu kitamsaidia kuandaa andalio la somo.

**Kielelezo Na. 8.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8.

Katika kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa alijibu kwa kuandika manufaa ya andalio la somo badala ya kueleza manufaa ya kitabu cha ziada katika ufundishaji wa somo la Kiswahili.


### 2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili

Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua kwa kifupi mambo manne ya kuzingatia katika uandishi wa lengo mahsusi. Watahiniwa 5,078, sawa na asilimia 100 waliofanya mtihani, walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yenye kiwango kizuri cha ufaulu, kwani asilimia 80.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Chati Na.5 inaonesha kuwa, watahiniwa 3,516, sawa na asilimia 69.2, walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani walipata alama 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na ujuzi wa kutosha katika mada ya *Maandalizi ya Kufundisha somo la Kiswahili*. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa ufupi mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuandika lengo mahususi. Mathalani, mtahiniwa mmoja katika kundi hili alitoa majibu kama vile: *Lengo mahususi liwe wazi, lioneshe muda wa kufikiwa, liwe linapimika na liwe linafikika.* Aidha watahiniwa waliopata alama 3 walitoa majibu kama vile: (a) *Yafikike- Malengo mahsusi yanapaswa kueleza namna ambavyo ni rahisi kuyafikia (b) Yapimike- Malengo mahsusi yanafaa pia kuwa yanapimika (c) Yaendane na somo- Malengo mahsusi yawe yanaendana na somo husika (d) Yawe wazi- Malengo mahsusi yanapaswa kuwa wazi kuelezea kitu gani kinatarajiwa*. Majibu hayo ya mtahiniwa yanaonesha kuwa kipengele (c) siyo sahihi. Kielelezo Na.9.1 ni sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9.


9 Malengo mahususi: Hiki ni kipengele muhimu ambacho kubeba jumla ya mambo yote ambayo mwanafunzi anapaswa kupata baada ya kipindi kimoja au zaidi.

Malengo mahususi lazima liwe na uhalisia; lendane na halisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Malengo mahususi yanatakiwa yafikike au kufikiwa baada ya mafunzo fulani.

Malengo mahususi lazima yapimike baada ya mafunzo.

Malengo mahususi lazima iwe na uhusika ambao wanafunzi ni kama walendaji wakuu katika zoezi la ufundishaji na ujifunzaji.

**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9.

Halikadhalika, watahiniwa 1,004, sawa na asilimia 19.8 ya waliojibu swali hili, walikuwa na uelewa mdogo kuhusu mambo yanayotakiwa kuzingatiwa wanapoandika lengo mahsusi, hivyo kupata alama 0 hadi 1.5. Baadhi ya watahiniwa hawakuelewa matakwa ya swali, badala ya kuandika mambo ya kuzingatia katika lengo mahsusi, watahiniwa hao waliandika hatua za kuzingatia katika andalio la somo kama vile: *Kuandika mada ndogo, Kuandika njia au mbinu zitakazotumika, kuandika hatua*

*utakazofuata na kuandika zana utakazotumia*. Katika kundi hili, baadhi ya watahiniwa waliandika vifaa anavyohitaji mwalimu anapoandaa Azimio la Kazi kama vile: *Kuwa na muhtasari wa somo la Kiswahili, Kuwa na vitabu vya kiada na ziada, Kuwa na vitabu au rejea mbalimbali*.

Aidha watahiniwa wengine waliandika mambo anayotakiwa kuandaa mwalimu kabla ya kuingia darasani. Mathalani, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yafuatayo: *Kuandaa andalio la somo, Kuandaa azimio la kazi, Kuandaa zana za ufundishaji, Kuandaa nukuu za somo*. Zaidi ya hayo, baadhi ya watahiniwa waliandika mambo ya kuzingatia mwalimu anapoandaa zana za kufundishia na kujifunzia kama vile: *(a) Idadi ya walengwa- Mwalimu anapoandaa malengo mahsusi anatakiwa ajue katika darasa langu nina wanafunzi wangapi (b) Umri na uelewa wa walengwa- Pia anapaswa ajue lengo mahsusi ninaloandaa linaenda kutumiwa na wanafunzi wa umri na uelewa gani (c) Maudhui ya somo- Kwa sababu unapoandaa lengo mahsusi unapaswa ujue unaenda kufundisha nini (d) Upatikanaji wa malighafi- Pia unapoandaa lengo mahsusi unapaswa kujua, je ni zana gani nitatumia ili niweze kukamilisha lengu langu.* Hii inadhihirisha kwamba watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo katika mada ya *Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili*. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza mambo ya kuzingatia unapoandika malengo mahsusi.

| 9 | i) Kusikiliza kwa umakini |
|---|---|
| | - Hii ni kwamba wakati wa maelekezo yanapotolewa - |
| | wanatakiwa kusikiliza kwa umakini ili kuweza kuelewa- |
| | vizuri. |
| | ii) Kuandika nukuu kidogo |
| | - Wakati maelekezo yanapotolewa ni muhimu kuandika nukuu |
| | kidogo kwa kuchukua hoja kuu zinazotolewa. |
| | iii) Kuzingatia matamshi ya mzungumzaji |
| | - Ili kuweza kuelewa vizuri ni muhimu kuzingatia |
| | matamshi ya mzungumzaji ili kupata ujumbe uliokusudi- |
| | wa. |
| | iv) Kubaini ujumbe ~~aliopo ko~~ walioupata |
| | - Wakati wanafundishwa kuhusu ~~upu~~ uandishi wa malengo |
| | mahususi mwanafunzi anatakiwa kubaini ujumbe alioupata |
| | kutokana na ufundishaji huo. |

**Kielelezo Na.9.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 9.


Kielelezo Na. 9.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeandika mambo ya kuzingatia wakati wa kusikiliza hadithi badala ya kuchambua mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuandika lengo mahsusi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 558, sawa na asilimia 11.0, walifanya swali hili na kupata alama 2.0 hadi 2.5. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya *Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili*, kwani waliweza kueleza kwa usahihi mambo mawili ya kuzingatia kama vile: *(a) Iendane na mada unayoenda kufundisha (b) Kumlenga mwanafunzi kama mtendaji mkuu (c) Kuzingatia umri na uwezo wa wanafunzi (d) Iendane na malengo ya somo.* Vipengele (a) na (b) ni majibu sahihi wakati (c) na (d) siyo majibu sahihi kwa sababu mtahiniwa aliandika mambo anayotakiwa kuzingatia mwalimu anapoandaa zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

### 2.1.10 Swali la 10: Upimaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza mambo manne yanayotakiwa kuwepo katika mwongozo wa usahihishaji. Watahiniwa 5,078, sawa na asilimia 100, walijibu swali hili, ambapo asilimia 92.2 walipata alama 2 hadi 4. Swali hili ni miongoni mwa maswali


yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 10 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 10*

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 3,936, sawa na asilimia 77.5, walijibu swali hili na kupata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Mada ya *Upimaji* hususani katika uandaaji wa mwongozo wa usahihishaji. Hivyo, waliweza kueleza mambo manne yanayotakiwa kuwepo katika mwongozo wa usahihishaji kama vile: *Jina la mtihani, mfano majibu ya mtihani wa Kiswahili darasa la tano, Idadi ya maswali yaliyopo katika mtihani mfano maswali 10, Alama za kila swali mfano swali la 1 jumla ya alama 6, Jumla ya alama zote za mtihani mzima, mfano, kama mtihani una alama 100 aoneshe.* Hata hivyo watahiniwa wengine walipata alama 3 kwa sababu waliandika mambo matatu kati ya manne ya kuzingatia au walitoa hoja nne, lakini kati ya hizo nyingine hawakuzitolea maelezo, hivyo kupata alama 0.5 badala ya alama 1. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *(a) Maswali (b) Majibu (c) Jina la mwalimu ili kujua ni mwalimu gani ameandaa mwongozo huo (d) Jina la somo ili kujua ni somo gani mfano kwenye mashule mengi ukute mfano mwalimu kaandaa mwongozo bila kuandika somo inakuwa vigumu walimu kujua ni somo gani.* Katika vipengele (a) na (b) mtahiniwa aliorodhesha mambo ya kuzingatia katika mwongozo badala ya kueleza kwa ufupi, hivyo kupata alama pungufu. Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha

sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza kwa ufupi mambo manne yanayotakiwa kuwepo katika mwongozo wa usahihishaji.


10

i) Majibu ya kila swali lililopo kwenye mtihani, hivyo mwalimu lazima aandae majibu ya kila swali lililopo kwenye mtihani.

ii) Alama au idadi ya alama za ufaulu kwa kila swali lililopo kwenye mtihani (maksi), hivy mwalimu lazima aweke ~~alama~~ idadi ya lama katikaa kila swali.

iii) ~~*~~ jina la somo, hivyo ni ~~[illegible]~~ muhimu mwalimu aandike jina la somo ili kuepuka mchanganyo na miongozo mingine ya usahihishaji wa mitihani.


iv) Muhula na mwaka, hivyo mwalimu anapaswe kuandika muhula na mwaka juu ya mwongozo wa usahihishaji.

**Kielelezo Na.10.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10.

Vilevile, watahiniwa 747, sawa na asilimia 14.7 ya waliojibu swali hili, walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya *Upimaji,* hivyo kueleza kwa usahihi hoja mbili kama vile: *(a) Majibu yaendane na swali, (b) jumla ya alama katika kila swali (c) Kuwepo kwa vitabu mbalimali vya rejea (d) kuzingatia maelezo ya wanafunzi katika usahihishaji*. Majibu ya mtahiniwa yanaonesha kuwa, vipengele (a) na (b) ni majibu sahihi ilhali (c) na (d) yalikosewa. Majibu hayo yanadhihirisha kuwa, watahiniwa katika kundi hili walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya *Upimaji*.

Hata hivyo, uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wachache (395), sawa na asilimia 7.8, walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao, walipata alama hafifu kwa sababu hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya *Upimaji*, hivyo walishindwa kueleza kwa ufupi mambo manne ya kuzingatia katika uandaaji wa mwongozo wa usahihishaji. Miongoni mwao waliandika vifaa vya mtaala kama vile: *Vitabu vya kiada, vitabu vya ziada, kiongozi cha mwalimu na kitabu cha mwalimu.* Aidha watahiniwa wengine walieleza vitu ambavyo mwalimu anaweza kuandaa kwa ajili ya kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji darasani. Majibu yafuatayo yalitolewa na

mtahiniwa mmoja katika kundi hili: *Kitabu cha kiada- Hiki ni kitabu kilichothibitishwa na taasisi yenye maswali na majibu, Kitabu cha ziada-Hiki ni kitabu kinachotumiwa na mwalimu ili kupata maarifa ya ziada, Kiongozi cha mwalimu- Hiki ni kitabu chenye maswali na majibu kilichoandaliwa ili mwalimu aweze kukitumia wakati wa kusahihisha, Nukuu za somo- Hizi ni nukuu zinazoandaliwa na mwalimu wa somo kila siku ili iweze kusaidia wakati wa kufundisha darasani.* Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa ufupi mambo manne yanayopaswa kuwepo katika mwongozo wa usahihishaji.


10

i) kujua maroal: yametoka katika mada gani

ii) kuzingatia Umri na Uelewa wa Wanafunzi.

iii) kujua idadi ya maswali.

iv) kuangalia Malengo yaliyowekwa.

**Kielelezo Na.10.2**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10.


Kielelezo Na. 10.2 ni majibu ya mtahiniwa ambaye aliandika mambo ya kuzingatia wakati wa utunzi wa maswali badala ya kueleza kwa ufupi mambo manne yanayopaswa kuwepo katika mwongozo wa usahihishaji.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha

Vilevile, ufaulu wa watahiniwa umegawanyika katika makundi matatu. Mtahiniwa alibainishwa kuwa na kiwango hafifu cha kufaulu endapo alipata alama 0 hadi 5.5, wastani endapo alipata alama 6 hadi 10 na alihesabika kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu iwapo alipata alama 10.5 hadi 15. Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) ya insha ambayo yalitungwa kutoka katika mada ya *Fasihi simulizi, Sarufi, Maandalizi ya kufundisha somo la Kiswahili* na *Upimaji.* Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali yote ambapo kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama sitini (60).

### 2.2.1 Swali la 11: Fasihi Simulizi

Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua sifa tano za mtambaji mahiri wa hadithi. Watahiniwa 5,078, sawa na asilimia 100 waliofanya mtihani, walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yenye kiwango kizuri cha ufaulu, kwani asilimia 72.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Watahiniwa 2,306, sawa na asilimia 45.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walipata alama 6.0 hadi 10.0 kutokana na uelewa wa wastani waliokuwa nao katika mada ndogo ya *Fasihi Simulizi*. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walichambua hoja mbili na kutoa maelezo yasiyojitosheleza. Aidha waliandika kwa usahihi utangulizi na hitimisho, hivyo kupata alama 6. Watahiniwa wengine walichambua hoja tatu zinazojitosheleza na kuandika kwa usahihi utangulizi na hitimisho, hivyo kupata alama 10. Mathalani, mtahiniwa mmoja alichambua hoja zifuatazo: *Mtambaji kulitawala jukwaa, kujivika sifa ya kitu anachokizungumzia, kufikisha ujumbe kwa njia ipasayo*. Aidha mtahiniwa mwingine alibainisha sifa zifuatazo: *Mtambaji kuwa na mpangilio mzuri wa visa na matukio, matumizi sahihi ya lugha na lafudhi yake pia kuwa na umahiri wa kujieleza*.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 1,419, sawa na asilimia 27.9 ya waliojibu swali hili, walipata alama 0 hadi 5.5 kwa

sababu walikuwa na uelewa mdogo katika mada ya *Fasihi Simulizi*. Watahiniwa hao walishindwa kuchambua umahiri aliokuwa nao mtambaji wa hadithi. Baadhi ya watahiniwa waliandika majibu yasiyokidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika mambo anayopaswa kuzingatia mwalimu anaposoma imla kama ifuatavyo: *Kuwa na usikivu, umahiri wa kuzingatia alama za uandishi, kuelewa hadithi katika mazungumzo, kutumia lugha fasaha, pia kufikiri kwa haraka*. Watahiniwa wengine hawakuelewa matakwa ya swali kwani badala ya kuchambua umahiri aliokuwa nao mtambaji wa hadithi, watahiniwa hao walichambua manufaa ya hadithi katika jamii. Mathalani, mtahiniwa mmoja aliandika majibu kama vile: *Kuelimisha jamii, Kukosoa jamii, Kuburudisha jamii, Kuonya jamii, Huasa jamii*.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wengine waliandika mazingira ambayo vivumishi hujitokeza katika sentensi kama vile: *Huweza kujitokeza baada ya nomino, Huweza kutumika katikati ya nomino, Huweza kuwakilisha kielezi katika sentensi, Huweza kutumika kuunganisha maneno katika sentensi, mfano, Mti <u>mrefu</u> sana, Huweza kutumika kuwakilisha idadi ya vitu fulani, wingi au uachache, mfano, maua <u>mazuri</u> yamechanua*. Majibu hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa hao hawakuelewa matakwa ya swali, pia hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya *Fasihi Simulizi*. Kielelezo Na.11.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuchambua umahiri aliokuwa nao mtambaji wa hadithi.

Hadithi ni habari fupi inayoelezea jambo fulani au
mbalo tayari yameshatokea katika mazingira
fulani. pia hadithi huweza kuwa na faida na
hasara kama itaeleweza katika madhara huatka
pia kuna ~~hadi~~ ~~arth~~ athiri ya kuangalia hadithi
katika televisheni mifano:

kusababisha mmonyoko wa maadili; kutokana
na kuangalia hadithi au kusikiliza hadithi kati
ka televisheni huweza kusababisha mmonyoko
wa maadili kwa vizazi vijavyo mfano msimuliaji
anaweza kutumia picha za uchi kuelezea

Huweza kusababisha ualifu wa mtandao
watu kuanza kutumia mtandao vibaya
na kuweza kuharibu lugha ya matusi au kusa
bisha kukosa na heshima

Ina gharama; katika hali hii sio wote wana
televisheni au wanaweza kulipia kuangalia
Sio wote ni vizuri kuwa tei hadithi huadithiwa
na mtu na pyo kwenye televisheni. pia huwe
za kutumiwa na wale wenye televisheni
tu.

Hupoteza muda mwingi kuangalia; mtu ana
kuwa bize kuangalia kuliko kufanya kazi
zake zingine za kawaida na pia husaba
bisha kuwepo kwa matabaka wa kujifunza
au kuangalia.

Huweza kusababisha migogoro; miongoni
mwa pande zote mbili mtu anaweza kuwa
anataka kumliki yeye mwenyewe kuliko
wengine au unakuta mtu anabadilisha bila

kuomba watu wengine kama yeye atakikua
ngalia. au kama amechoka wengine angalie
mpaka warithike na wao.

Hubabisha matabaka; hapo kuweza kuibua vitu
ndi mbalimbali mfano wale wenye televisheni
na wale ambayo hawana huanza kutengwa
wakaa wenyewe. pia sio wote wanajua kutu
mia televisheni kuna ~~wana~~mbayo hawajui ku
somo na kuandika. televisheni hutumiwa na
wanaojua kusoma na kuandika.

Hivyo; Hadithi huwaidia kukuza msamiati
katika lugha ya kiswahili, kuelimisha, kubura
disha jamii, kukosoa, kutoa elimu kuanzia kiza
zi kimoja hadi nyingine kwa kubadilishana
maudhui yanayotokana na hadithi yale mazuri
zaidi.

**Kielelezo Na.11.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 11.

Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika madhara ya kusikiliza hadithi kupitia televisheni badala ya kuchambua umahiri aliokuwa nao mtambaji wa hadithi kwenye kipindi cha “Hadithi Zetu”.

Kwa upande mwingine, uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 1,353 (26.6%) walijibu swali hili na kupata alama 10.5 hadi 15. Watahiniwa hao, walikuwa na umahiri na maarifa ya kutosha katika mada ya *Fasihi simulizi* kwa sababu waliweza kuchambua sifa za mtambaji mahiri wa hadithi kupitia kipindi cha “Hadithi Zetu” kilichorushwa katika televisheni ya taifa. Miongoni mwa majibu yaliyotolewa na watahiniwa hao ni kama vile: *Mtambaji alikuwa mahiri wa lugha ili atambe hadithi bila kusitasita, Mtambaji alikuwa na uwezo wa kushirikisha hadhira yake kwa kuwauliza maswali, Mtambaji alikuwa na uwezo wa kuigiza baadhi ya mambo kwa kutumia ishara, Mtambaji alikuwa mcheshi kwa kuhusisha mambo yanayochekesha hadhira ili kuburudisha hadhira yake, Mtambaji alikuwa na uwezo wa kudadisi namna hadithi yake ilivyopokelewa.* Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika kwa usahihi sifa za mtambaji mahiri wa hadithi.


11

Hadithi. Ni tungo au tanzu ya fasihi simulizi inayotumia lugha nathari yaani lugha yenye mjazo wa maongezi ya kila siku. Hadithi huwa na vipera vyake ambavyo ni pamoja na ngano, visakale, visasili, vigano na soga, hivyo kila kipera cha hadithi kina maana yake mfano tarihi au visakale hizi husimulia matukio maalumu ya kihistoria wakati soga hizi ~~husimu~~ ni hadithi fupi za kukejeli na kuchekesha. Hivyo ili hadithi iweze kuvutia kwa hadhira ni muhimu kuzingatia mambo mbalimbali wakati wa utambaji wake. Hivyo mtambaji alikuwa na umahiri ufuatao uliomsababisha Johari kufikiri kuwa "Si kila mtu anaweza kuwa mtambaji wa hadithi"

Matumizi ya vitendo wakati wa utambaji. Hadithi huwa inamtaka mtambaji aweze kutumia vitendo pale inapotakiwa mfano ikiwa ni kitu cha kushangaa basi aoneshe hali au tendo la kushangaa au mfano ni kitu kili chokuwa kinatisha kwenye hadithi aoneshe namna ya vitisho aidha kwa kufungua mdomo au kutisha kwa kutumia miguu a mikono.

Mtambaji alitumia wahusika kama ndege, wanyama, miti, mazimwi; Ili hadithi iweze kuvutia ni muhimu pawe na wahusika kama ambao nilio wataja, na wakati mwingine wahusika hao hupewa uwezo ambao hawana mfano kwenye hadithi mtambaji anaweza akasema "kisha mti ukasema" ambavyo kiuhalisia mti hauwezi kuongea hivyo huo ni umahiri ambao Johari ~~anaweza~~ aliuona, yaani kuvipa uwezo vitu ambavyo ~~a~~ haviwezi kufanya hivyo

Mtambaji alizingatia mianzo na miisho ya hadithi. Ili umahiri wa mtambaji wa hadithi uonekane ni muhimu pawe na mianzo yaani hadithi ifeleweke kwa hadhira kuwa imeanzia wapi lakini pawe na miisho yaani hadhi-



11 Cont.

a ra aelewe mwisho wa hadithi, kwani Pasipo kuzi
ngatia hayo Mtambaji hawezi kuwa na Umahiri wa
kutamba hadithi.
Mtambaji kutumia Matukio mengi madogo
madogo ambayo baadaye hujenga tukio moja kuu. Umahi
ri pia ambao aliona Johari ni Pamoja na kugundua
kuwa mtambaji au katika hadithi kulikuwa na matukio
madogo-madogo ambayo yamejenga tukio moja kuu kwani
kama siyo mahiri mtambaji hawezi kuwa na uwezo
huo wa kutumia matukio madogomadogo na kuunda
tukio moja kuu.
Mtambaji kuhusisha tanzu nyingine za fasihi sim-
ulizi. Hadithi inaruhusu kuhusisha tanzu nyingine za fasi
hi simulizi mfano mtambaji anaweza akatumia maigizo,
nyimbo na mashairi wakati wa utambaji wake, hivyo iki
wa mtambaji hawezi kughani shairi umahiri wake hauwe
zi kuonekana au ikiwa hawezi kuimba mtambaji huyo
hana umahiri. Hivyo Johari aliona umahiri wa mtamba
ji kwa kuwa aliweza kuhusisha tanzu nyingine za fasihi
simulizi.
Hivyobasi, ni muhimu kutazama vipindi mbali
mbali vya hadithi au kupitia au kusoma vitabu vya hadi
thi kwani hadithi huwa na funzo kwa jamii hivyo husai
dia kuitoa jamii sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

**Kielelezo Na.11.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 11.

### 2.2.2 Swali la 12: Sarufi

Swali lilimtaka mtahiniwa akubaliane, kwa kutumia hoja tano, na kauli isemayo "Kivumishi ni aina mojawapo ya maneno inayojitokeza katika mazingira tofauti tofauti katika sentensi". Watahiniwa 5,078, sawa na asilimia 100, walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yenye kiwango cha wastani cha ufaulu kwani asilimia 67.6 ya watahiniwa walipata alama 6.0 hadi 15 kama inavyoonekana katika chati Na.12.





**Chati Na. 12**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12*

Karibu nusu ya watahiniwa wote (2,519), ambao ni sawa na asilimia 49.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walipata alama 6.0 hadi 10.0 kwa sababu walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya *Sarufi*. Katika kundi hili wapo watahiniwa waliotoa hoja mbili zisizojitosheleza na kuandika kwa usahihi utangulizi na hitimisho, hivyo kupata alama 6.0. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja tatu zinazojitosheleza na kuandika kwa usahihi utangulizi na hitimisho, hivyo kupata alama 10.0. Majibu hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na umahiri wa wastani katika mada ya *Sarufi.*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,643 (32.4%), walipata alama 0 hadi 5.5 kwa sababu hawakuwa na umahiri wa kutosha katika mada ya *Sarufi* kipengele cha *aina za maneno*. Watahiniwa hao walishindwa kutoa kauli tano za kukubaliana kwamba kivumishi ni aina mojawapo ya maneno inayojitokeza katika mazingira tofauti tofauti katika sentensi. Miongoni mwao waliandika kuhusu mambo anayopaswa kuzingatia msimuliaji wa hadithi kama vile: *Kuzingatia mpangilio wa visa na matukio, kuzingatia ujumbe uliokusudiwa katika jamii, kuzingatia muda wa usimuliaji, Kuzingatia wahusika na muda wa usimuliaji*. Aidha, watahiniwa wengine waliandika mambo ya kuzingatia unapotunga maswali ya insha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *Maswali ya insha yaendane na umri, Maswali ya insha yawe yapo wazi na kueleweka, Wakati wa kutunga maswali ya insha tuepuke kidokezo cha majibu, Tunapotunga maswali ya insha tuhakikishe tumetumia lugha fasaha.* Hali kadhalika, baadhi ya watahiniwa walipata alama 0 kwa sababu hawakujibu chochote. Hii inaonesha

kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya *Sarufi* hususani kwenye kipangele cha *aina za maneno*. Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.


12

Kivumishi ni aina ya maneno ambayo husimama badala ya nomino. "Kivumishi ni aina mojawapo ya maneno inayojitokeza katika mazingira tofauti katika sentensi". Nakubaliana na kauli hii kwa kuwa hoja zifuatazo.

Huvumisha kuhusiana na jambo: Kivumishi huweza kuvumisha kuhusu jambo fulani ama kitu kuhusiana na kitu fulani hivyo kivumishi inaweza kujitokeza katika mazingira tofauti katika sentensi kwa kuvumisha kuhusiana na jambo fulani.

Husimama badala ya nomino/jina; Kivumishi pia husimama badala ya nomino/jina katika sentensi ambapo inasimama aupasimama nomino nakuweza kusimama yenyewe badala ya nomino mfano Wote wametoka shule neno wote ambapo ni kivumisha ambayo ilitakiwa isimame Wanafunzi wametoka shule badala yake neno wote linavumisha au limesimama badala ya nomino hivyo basi Kivumishi Kinaweza kujitokeza katika Mazingira tofauti katika sentensi

Huonesha nafsi katika sentensi; pia kivumishi kinatokea kwenye sentensi kwa kuonesha nafsi ambayo husimama kama kivumishi ambapo kivumishi kinaonesha nafsi kwenye sentensi kwa kuonesha nafsi kwenye sentensi mfano Yeye analima ambapo yeye ni nafsi ambayo ipo kwenye sentensi kama kivumishi hivyo basi kivumishi kinaweza kujitokeza katika mazingira tofauti katika sentensi.

**Kielelezo Na.12.1**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 12.

Katika kielelezo Na.12.1 mtahiniwa alieleza umuhimu wa kivumishi katika sentensi badala ya kuonesha mazingira tofauti tofauti ambamo kivumishi hujitokeza.

Hata hivyo, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 916, sawa na asilimia 18.0, walijibu swali hili na kupata alama 10.5 hadi 15.0. Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Sarufi* kipengele cha *aina za maneno*. Hivyo, waliweza kutoa hoja tano kwa usahihi ili kukubaliana na kauli kuwa kivumishi ni aina mojawapo ya maneno inayojitokeza katika mazingira tofauti tofauti katika sentensi. Mojawapo ya majibu waliyoandika ni kama vile: *Vivumishi vya sifa, mfano Maua meupe yamenyauka. Vivumishi vya idadi; mfano viti vitatu vimevunjika. Vivumishi viulizi; mfano Mbwa yupi amepotea? Vivumishi vya A-unganifu; mfano kioo ambacho kimepotea kimeonekana. Vivumishi vimilikishi; Nyumba yangu imebomolewa*. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya majibu sahihi ya mmojawapo wa watahiniwa.

12

Kivumishi; ni mojawapo ya aina za maneno ambayo hueleza zaidi kuhusu nomino na kiwakilishi. Mara nyingi kivumishi huvumisha sifa ya kitu. Naku baliana na kauli isemayo kivumishi ni aina mojawapo ya maneno inayojitokeza katika mazingira tofauti tofauti katika sentensi kutokana na aina zake. Zifuatazo ni aina za vivumishi:-

Kivumishi cha sifa; Aina hii ya kivumishi hueleza sifa ya kitu au mtu

Mfano Mtoto mzuri amekuja. Neno mzuri ni kivumishi na hueleza uzuri alionao mtoto.

Vivumishi vya idadi; Vivumishi vya namna hii hueleza idadi kamili ya vitu, wala hivyo hutumika mwanzoni mwa sentensi


Mfano <u>Watano</u> wamenusurika ajali
V

Vivumishi vimilikishi; Hii ni aina ya vivumishi ambavyo huonyesha hali ya umiliki wa kitu au nyumba na hata binadamu.

Mfano - mazingira <u>yetu</u> ni mazuri
V

→ Cheo <u>chetu</u> kimeshindikana.
V

Vivumishi viulizi; Ni aina ya vivumishi ambavyo huuliza mambo au jambo flani kiundani kwa lengo la kutaka kujua ukweli halisi.


12 Cont.

mfano → Wangapi wameondoka?

→ Wangapi wameripoti shule?

Vivumishi vya wakati au muda: Vivumishi vya namna hii hutumika kuonyesha muda ambao tendo limefanyika

mfano → Baba aliondoka Alfajiri

→ Waliwasili kitipunde.

Vivumishi vya a-unganifu: Aina hii ya vivumishi huweza kutumia namba kama la-saba, wa-ngapi na la-nne ambayo huambatanisha kilabi.


mfano → la-saba wamefaulu.

Hivyo: Vivumishi huweza kutokea sehemu yoyote katika sentensi kwa sababu ya aina ~~mali~~ mbalimbali za vivumishi na tabia zake pia.

Kielelezo Na.12.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 12.

### 2.2.3 Swali la 13: Maandalizi ya Kufundisha


Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua mambo yanayofanyika katika kila hatua ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, yaani katika utangulizi, maarifa mapya, tafakuri na hitimisho. Watahiniwa 5,078, sawa na asilimia 100, walijibu swali hili, ambapo asilimia 97.7 walipata alama 6.0 hadi 15.0. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 13 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 13*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, zaidi ya nusu ya watahiniwa (3,386), sawa na asilimia 66.7, waliojibu swali hili walipata alama 10.5 hadi 15.0 kwa sababu walikuwa na umahiri wa kutosha katika mada ya *Maandalizi ya Kufundisha.* Watahiniwa waliopata alama 15.0, waliweza kuchambua kwa usahihi mambo yanayofanyika katika kila hatua katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichambua mambo kama vile: *Utangulizi, katika hatua hii mwalimu anaweza kutumia mbinu kama kuuliza maswali ya chemsha bongo, kutumia bungua bongo ili kupata maarifa ya awali au kufanya marudio ya somo lililopita; Katika hatua ya maarifa mapya mwalimu anaanza kuwaongoza au kuwezesha wanafunzi juu ya jambo linalotakiwa kufundishwa; Katika tafakuri mwalimu hutakiwa kutafuta ufanisi wa kile alichofundisha kwa kuuliza maswali yatakayomwongoza mwanafunzi kutoa mrejesho wa somo; Hitimisho ni hatua ambayo hufanyika mwishoni mwa somo, mwalimu huweza kutoa muhtasari wa somo mwenyewe au kuuliza wanafunzi mmoja mmoja.* Kielelezo Na. 13.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi swali hili.

13 Ufundishaji: Ni kitendo cha kutoa maarifa, stadi na muele-
keo kwa mtu fulani au ni kitendo cha mwalimu kutoa
maarifa stadi mbalimbali na muelekeo kwa wanafunzi
wake.
Ujifunzaji: Ni kitendo cha kupokea maarifa stadi na
muelekeo kutoka kwa mtaalamu au mwalimu / kutoka
kwa mtu yeyote mwenye ujuzi.
"Ufundishaji na ujifunzaji ni mchakato unaojumuisha hatua
ya utangulizi, maarifa mapya, tafakuri na hitimisho" yafuatayo
ni mambo yanayofanyika katika kila hatua.
Utangulizi: hii ni kipengele cha kwanza ambayo mwali-
mu hutumia maswali ya bunguza bongo, maswali na majibu,
Nyimbo katika kuwaweka wanafunzi wake kuwa tayari
kwa ajili ya kujifunza pia katika kipenge hiki mwalimu
anaweza kufanya mapitio ya kazi / zoezi alitoa
kwa wanafunzi wake lakini anaweza kutumia maswali
ya udadisi kabla ya kuanza kufundisha kutaka kujua maari-
fa ya awali waliyonayo wanafunzi wake kuhusu mada ambayo
anayekwenda kufundisha mfano katika kipengele hiki
mwalimu anaweza kutumia maswali yafuatayo kudadisi
wanafunzi wake ili kujua maana ya kile anachoenda kufundi-
sha pamoja zake umuhimu
Maarifa mapya: Mwalimu wa somo katika kipengele
hiki anatakiwa kufanya yafuatayo: kutambulisha mada atakaye-
ye fundisha, mada ndogo atakayo fundisha kwa wakati huo
na kuweza kutumia mbinu mbalimbali ili kuweza kujenga
a wanafunzi wake uwezo wa kumudu somo hilo. mbinu
hizo ni kama vile onesho mbinu, majadiliano ya vikundi
maswali na majibu ili wanafunzi wake waweze kupata
maarifa na stadi alizotarajia kuwafikishia / kuwafundi-
sha. ili wanafunzi waweze kuwa na uwezo wa kupata
kumbukumbu za kudumu. Kuhusu umahiri mahususi


13 Cont.

Tafakuri: hii ni kipengele ambayo mwalimu ataandika mawazo kutoka kwa wanafunzi wake baada ya kumaliza kipindi chake: maoni/mawazo hayo ni kama vile wanafunzi wameweza kulielewa somo kutokana na mbinu shirikishi nilizotumia katika ufundisha. pia mwalimu anaweza kuandika kama wanafunzi wameelewa na kufurahia somo lake na kama zana au mbinu aliyotumia kufundisha wanafunzi wanapenda.

Hitimisho: Hiki ni kipengele cha mwisho katika ufundishaji na ujifunzaji ambayo mwalimu wa somo anaweza kuhitimisha somo lake kwa njia mbalimbali. Kwa mfano mwalimu anaweza kuhitimisha somo kwa kuliza maswali; kutoa zoezi kwa wanafunzi; kusikiliza maoni ya wanafunzi baada ya kipindi na kusahihisha kazi ya wanafunzi;

Hivyo basi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji mwalimu anatakiwa kuweza kufuata hatua zote za ufundishaji na ujifunzaji ili kuweza kuwa na mtiririko mzuri wa mawazo/mantiki katika ufundishaji wake ili kuwajengea wanafunzi wanafunzi kumbukumbu za kudumu.

**Kielelezo Na. 13.1**: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 13.


Aidha, watahiniwa 1,573, sawa na asilimia 31, walijibu swali hili na kupata alama 6.0 hadi 10.0. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya *Maandalizi ya Ufundishaji*. Kwa mfano, miongoni mwao walipata alama 6.0 kwa sababu waliweza kuandika utangulizi, hitimisho na kuchambua hoja zote nne lakini walishindwa kuzieleza kwa ufasaha. Zaidi ya hayo, watahiniwa waliopata jumla ya alama 10.0, waliweza kuandika utangulizi na kuchambua hatua tatu kwa usahihi kati ya nne zilizotakiwa.

Kwa upande mwingine, uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wachache (119), sawa na asilimia 2.3, walipata alama 0 hadi 5.5. Watahiniwa hao, walipata alama za kiwango hafifu kwa sababu hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya *Maandalizi ya Ufundishaji,* hivyo walishindwa kuchambua mambo yanayofanyika katika hatua ya *utangulizi, maarifa mapya, tafakuri* na *hitimisho* wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Miongoni mwao waliandaa andalio la somo na kubainisha kazi za mwalimu (mfano: *Mwalimu atawaongoza wanafunzi kuimba wimbo*) na mwanafunzi

(*wanafunzi wataimba wimbo*) wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji .

Watahiniwa wengine waliandika kuhusiana na mambo ambayo mwalimu anaweza kuandaa kabla ya kuingia darasani kama vile: *Kuandaa zana za kufundishia, kuandaa nukuu za somo, kuandaa azimio la kazi, kuweka bayana mada ndogo na mada kuu, kuweka wazi walengwa wa somo*. Aidha watahiniwa wengine waliandika utangulizi peke yake na kupata alama 1. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *Ufundishaji ni kitendo cha kusafirisha maarifa kutoka kwenye chanzo kwenda kwa mwanafunzi. Zifuatazo ni baadhi ya mambo ya kuzingatia katika shughuli za ufundishaji na ujifunzani*.

Zaidi ya hayo, watahiniwa wengine walitoa majibu yasiyohusiana na matakwa ya swali kama vile: *Utangulizi ni stadi inayotumia maneno ili yaweze kuleta maana ya kitu, kanuni za utungaji lugha fasaha, matumizi sahihi ya uandishi na alama za uandishi: Katika hatua ya utangulizi, maarifa mapya, tafakuri na hitimisho utazingatia kuuliza maswali, umahiri ulioandaliwa kufundishwa, zana zilizotumika, kutoa zoezi na kusahihisha*. Kielelezo Na.13.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.



13 Cont.
hii kupima uelewa wa mwanafunzi
Humsaidia mwalimu kuandika
mawazo ya wanafunzi; mfano wanafunzi
walioelewa na ambao hawajaelewa kw
a kuwa uliza wanafunzi kutokana
na mada iliyofundishwa hii ni mambo
yanayofanyika katika hatua za ujifunzaji
katika hatua ya tafakuri ni kuele
zea mafanikio na kutofanikiwa kwa
maudhui kwa kuwauliza wanafunzi.
Humsaidia mwanafunzi kukuza kipaji;
mfano mwanafunzi anapopata maarifa mapya
juu ya kudhibiti majanga huendelea kukuza
kipaji cha mwanafunzi kutokana na istila
hi ya mwanafunzi hii ni mambo ya yanayo
fanywa katika hatua za ufundishaji kwa
kupima na kukuza vipaji kwa kuongezea
marifa mapya.
Mambo ya kuliza maswali kwa uelewa
wa kupima; mfano kupima istilahi ya
kuandika mfano wa hatua ya
kutumia umahiri huweza kupima
istilahi ya mwanafunzi kuweza
kuandika kwa ufasaha.
Kwahiyo; Mwalimu na mwanafunzi
kuweza kujifunza hatua za ujifu
nzaji na ufundishaji katika andalio
la somo kwa kupima mambo
muhimu katika utendaji wa hatua
hiyo mfano matumizi ya umahiri
hitimisho la somo.

**Kielelezo Na. 13.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 13.

Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza manufaa ya hatua alizopewa kuchambua (utangulizi, maarifa mapya, tafakuri na hitimisho) badala ya kuchambua mambo yanayofanyika katika kila hatua wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.2.4 Swali la 14: Upimaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua mambo sita ambayo mwalimu Hamisi anapaswa kuzingatia anapotunga maswali ya insha. Asilimia 100 ya watahiniwa (5,078) waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yenye kiwango kizuri cha ufaulu kwani asilimia 76.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 6.0 hadi 15.0 kama inavyoonekana katika Chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14*

Chati Na.14 inaonesha kuwa, watahiniwa 3,386, sawa na asilimia 41.6, waliojibu swali hili walipata alama 10.5 hadi 15.0. Ufaulu huo unadhihirisha kuwa walikuwa na umahiri wa kutosha katika mada ya *Upimaji*. Watahiniwa wa kundi hili, waliweza kuchambua mambo manne hadi sita ambayo mwalimu Hamisi anapaswa kuzingatia anapotunga maswali ya insha. Mathalani, mmoja wa watahiniwa hao aliyechambua hoja sita aliandika kama ifuatavyo: *Kutumia lugha isiyo na utata katika kuuliza maswali ya insha, kuepuka kutumia misamiati migumu katika kuuliza maswali ya insha, kutunga maswali kulingana na kiwango cha elimu ya mwanafunzi, kuhakikisha kuwa kila swali lina maelezo muhimu juu ya mipaka ya majibu, kutunga maswali yanayopima kiwango cha juu cha maarifa pia kuandaa majibu ya maswali ili kuweza kusahihisha mawazo ya wanafunzi*.

Aidha watahiniwa waliopata alama 10.5 waliandika kwa usahihi utangulizi, hitimisho na kutoa hoja nne zinazojitosheleza kama vile:

*Maswali yaendane na mada zilizofundishwa, Kuzingatia umri wa wanafunzi, Maswali yasiwe marefu na yasijirudie, Kuwe na muda mrefu wa kujieleza*. Kielelezo Na. 14.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.


**14** Maswali ya insha: Ni aina ya maswali ambayo humtaka mwanafunzi ajenge hoja na kuweza kujieleza katika mtindo wa aya. Zipo aina mbili za maswali ya insha nazo ni maswali ya insha yenye ukomo na maswali ya insha yasiyo na ukomo.

Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia wakati wa kutunga maswali ya insha.

Kwanza kabisa uzingatie uelewa wa wanafunzi katika kutumia msamiati wa lugha. Mfano unapotunga maswali ya insha kwa wanafunzi wa darasa la tano, misamiati itakayotumika ni tofauti na ile ya darasa la saba kwa uelewa wa kupambanua msamiati hiyo unatofautiana.

Kadhalika pia uzingatiaji wa ukomo wa swali. Hii ina maana kwamba swali liwekwe wazi hoja idadi ya hoja zinazotakiwa ziandikwe katika swali. mfano: "Fafanua aina tano za maneno unazozifahamu" Swali hili lina ukomo kwani limeonesha kabisa mwanafunzi aandike aina tano tu za maneno.

Si hivyo tu bali utungaji wa maswali ya insha ni muhimu kuzingatia uwazi. Swali liweke wazi kile kitachoulizwa au kinachopaswa kujibiwa. mtungaji aepuke kutumia maneno mengi yanayoweza kuficha swali. mfano: "Eleza kwa kutoa mifano ya kutosha ngeli (6) za maneno. Swali hili halijawekwa wazi kinachotakiwa kujibiwa ni ngeli.





**Kielelezo Na. 14.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 14.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 1,754, sawa na asilimia 34.5 ya waliojibu swali hili, walipata alama 6.0 hadi 10.0 kwa sababu walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya *Upimaji*. Watahiniwa hao waliweza kutoa hoja tatu hadi nne kati ya sita walizotakiwa kueleza kuhusu mambo ya kuzingatia katika utungaji wa maswali ya insha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliyepata alama 6 alichambua mambo kama vile*: (a) Maswali ya insha lazima yawe ni yenye kufikirisha (b) yazingatie kiwango cha elimu (c) yazingatie mada zilizofundishwa (d) yasiwe na dalili au viashiria vya kumpa mwanafunzi majibu (e) yalenge kupima maarifa ya mwanafunzi (f) yasiwe ni yenye kujirudia rudia.* Katika majibu hayo, kipengele (b), (c) na (d) ni hoja sahihi wakati (a), (e)

na (f) siyo sahihi. Aidha watahiniwa waliopata alama 10 waliandika kwa usahihi utangulizi, hitimisho na kutoa hoja sita ambazo baadhi yake zilikuwa zinazojitosheleza wakati nyingine zilikosa maelezo fasaha, hivyo kupata alama pungufu.

Hata hivyo, uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 1,108, sawa na asilimia 23.9, walipata alama 0 hadi 5.5. Watahiniwa hao, walipata alama za kiwango hafifu kwa sababu hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya *Upimaji* na hivyo kushindwa kueleza mambo ya kuzingatia katika utunzi wa maswali ya insha. Watahiniwa wengi walichanganya kwa kuandika mambo ya kuzingatia katika utunzi wa insha badala ya utunzi wa maswali ya insha kama vile: *Mada inayozungumziwa, Matumizi ya alama za uandishi, matumizi sahihi ya lugha fasaha, Mtirirko sahihi wa matukio na Mawazo makuu.* Aidha watahiniwa waliopata alama 5 waliweza kuandika utangulizi na kutoa hoja mbili sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo: *(a) Kuzingatia uelewa wa wanafunzi (b) Kuzingatia umri wa wanafunzi (c) Kuzingatia maudhui yanayopimwa (d) Kuzingatia idadi ya walengwa (e) Kuzingatia lugha fasaha*. Hoja (c) na (e) katika majibu hayo ni sahihi ilhali hoja (a), (b) na (d) siyo sahihi. Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa usahihi mambo ya kuzingatia katika utunzi wa maswali ya insha.


14

Insha ni mtiririko au hoja ilizopangwa mpangilio maalumu wenye kuleta maana katika kupeleka ujumbe.

Zingatizo ni sifa anayopaswa kuyazingatia katika uandaji wa kazi hiyo

- Kichwa cha insha; katika uhandisi wako anapaswa kuzingatia kichwa cha insha ili kujua kinaeleza nini kuhusu insha na kukupa muongozo wa kujibu maswali hayo.
- Mwanzo wa insha; Insha inapaswa kuwa na mwanzo mzuri wenye kuwa na vielelezo na maelezo mazuri kwa msomaji kuelewa
- Kiini cha insha:; kiini cha insha huwa kinaeleza zaidi kuhusu insha inataka nini na inahusiana na nini
- Mwisho au hitimisho; Huu ni mwisho wa insha anapaswa kuzingatia mbinu wa insha.

**Kielelezo Na. 14.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 14

Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha badala ya mambo ya kuzingatia katika utunzi wa maswli ya insha.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA

Mtihani wa Cheti cha Ualimu Daraja la A wa Somo la Kiswahili ulikuwa na maswali 14 yaliyotungwa kutoka katika mada 7. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa walifanya vizuri katika mada nne ambazo ni sawa na asilimia 57.1 ya mada zote zilizotahiniwa. Mada hizo ni: *Vifaa vya mtaala* (97.8%), *Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili* (88.9%), *Fasihi Simulizi* (82.3%), na *Upimaji* (84.2%). Mada hizo zilikuwa na ufaulu wa kiwango kizuri kwa sababu watahiniwa wengi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada husika na kuelewa matakwa ya kila swali. Aidha, waliweza kujieleza kwa ufasaha na kufuata taratibu na kanuni za uandishi hasa katika maswali ya insha.

Vilevile, watahiniwa walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu katika mada tatu ambazo ni sawa na asilimia 42.9 ya mada zilizotahiniwa. Mada hizo ni: *Sarufi* (65.4%)*, Stadi za Lugha* (61.4%) na *Utungaji* (57.2%).

Uchambuzi zaidi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada zilizotahiniwa unaonesha kuwa hakukuwa na mada iliyokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu.

Aidha, kiwango cha ufaulu kimeongezeka katika mada za *Utungaji, Fasihi Simulizi, Vifaa vya Mtaala* na *Maandalizi ya Kufundisha somo la Kiswahili.* Kwa mwaka 2022 mada hizo zilikuwa na ufaulu wa asilimia 55.0, 48.1, 82.5 na 58.1 na mwaka 2023 asilimia 57.2, 82.3, 97.8 na 88.9 mtawalia. Vilevile, kiwango cha ufaulu kimeshuka katika mada za *Upimaji, Sarufi* na *Stadi za lugha*. Kwa mwaka 2022 mada hizo zilikuwa na ufaulu wa asilimia 99.4, 88.2 na 79.9 na mwaka 2023 asilimia 84.2, 65.4 na 61.4. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2023 kimeshuka kwa asilimia 0.12 ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo watahiniwa walifaulu kwa asilimia 100.

## 4.0 HITIMISHO

Taarifa hii inaonesha kuwa, watahiniwa wamefaulu kwa kiwango kizuri katika somo la 621 Kiswahili kwa mwaka 2023 kwani asilimia 99.88 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walifaulu. Aidha, watahiniwa wamefaulu kwa kiwango hicho kwa kuwa walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa na pia kuelewa matakwa ya maswali mbalimbali.

Licha ya watahiniwa kufaulu kwa kiwango cha juu, juhudi zinahitajika katika kuimarisha uelewa wa mada zilizokuwa na ufaulu wa wastani ambazo ni: *Sarufi, Stadi za lugha* na *Utungaji* ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kwa mitihani ijayo.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ufaulu wa watahiniwa katika somo la 621 Kiswahili ulikuwa mzuri kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali, wadau mbalimbali wa elimu pamoja na wakufunzi katika kuhakikisha kuwa kiwango cha umahiri kinaongezeka. Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika somo hili, inashauriwa kwamba:

(a) Katika mada ya «*Utungaji»*, walimu tarajali wapewe mazoezi ya kutosha ya kuandika insha zinazohusiana na mada mbalimbali, kwa mfano, elimu ya mazingira, usawa wa jinsia, rushwa, madawa ya kulevya na ajira kwa watoto.

(b) Walimu tarajali wapewa mazoezi ya kutosha ya kusikiliza ambayo yatawaongezea maarifa na uelewa wa mambo ya kuzingatia wanaposikiliza mazungumzo au masimulizi na hivyo kuwa mahiri katika stadi hiyo.

(c) Kwa upande wa mada ya «*Sarufi*» , wakufunzi watumie mbinu mbalimbali zitakazowawezesha walimu tarajali kuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na mada hiyo. Mbinu watakazotumia ni pamoja na : vikundi vya majadiliano kuhusu aina za maneno katika lugha ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na kutoa mazoezi ya kutunga sentensi mbalimbali zenye kauli za utendaji.

**KIAMBATISHO CHA PEKEE**

## UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

| Na | Mada | Namba ya swali | Viwango vya Ufaulu (%) | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 40 na Zaidi | Wastani | |
| 1. | Vifaa vya mtaala | 8 | 97.8 | 97.8 | vizuri |
| 2. | Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili | 13 | 97.7 | 88.9 | Vizuri |
| | | 9 | 80.2 | | |
| | | 14 | 76.1 | | |
| 3 | Fasihi Simulizi | 4 | 98.6 | 82.3 | Vizuri |
| | | 6 | 76.1 | | |
| | | 11 | 72.1 | | |
| 4 | Upimaji | 10 | 92.2 | 84.2 | Vizuri |
| | | 14 | 76.1 | | |
| 5. | Sarufi | 12 | 67.6 | 65.4 | Wastani |
| | | 2 | 63.2 | | |
| 6. | Stadi za lugha | 1 | 63 | 61.4 | Wastani |
| | | 5 | 59.8 | | |
| 7. | Utungaji | 3 | 98.6 | 57.2 | Wastani |
| | | 7 | 15.8 | | |